# THE MWALIMU NYERERE FOUNDATION

# HOTUBA YA DK. SALIM AHMED SALIM, MWENYEKITI, TAASISI YA MWALIMU NYERERE, WAKATI WA KUFUNGA TAMASHA LA PILI LA TAASISI NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

*Dar es Salaam`*
***19 Julai 2002***

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bibi Maria Shaba,

Mheshimiwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANGO,
Bibi Mary Mwingira,

Waheshimiwa Viongozi Mbalimbali wa Serikali na Mashirika Yasiyo ya Serikali,

Waheshimiwa Wageni Waalikwa na Washiriki Wote,

Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa naomba niwashukuru Viongozi wa TANGO kwa kunialika kuja kushiriki katika awamu ya mwisho ya Tamasha lenu. Wajibu mlionipa ni mdogo lakini ni mzito. Nasema ni mdogo kwani kazi yote imeshafanywa na ninyi wenyewe washiriki wa Tamasha hili katika siku nne hizi ambazo mmekuwa mnajadiliana mambo mbalimbali ambayo ndiyo yamekuwa ni Agenda ya Tamasha lenu. Lakini hapo hapo ni nzito na kwa kiwango fulani ni ngumu kwa sababu kwa vile mimi sikushiriki katika Tamasha lazima nitahadhari ili katika hotuba yangu ya ufungaji nisianzishe mjadala mpya.

Kwa kuzingaita hali hii nadhani mtanielewa na mtanisamehe kama katika hotuba yangu nitarejea au kuelezea mambo ambayo au mmeshayazungumza au mnayaelewa vyema wala hamhitaji kukumbushwa.

Ningependa kuanza kwa kuainisha jambo ambalo ni la wazi. Nalo ni kwamba Tamasha lenu hili limefanyika katika wakati muwafaka na limezingatia baadhi ya masuala ambayo yana umuhimu kwa Taifa letu na pia kwa bara letu kwa jumla. Kuhusu wakati ni jambo la kuridhisha na kutia moyo kwamba kila siku zikisonga mbele nchi nyingi zaidi za Afrika zinaelewa na kuthamini mchango muhimu wa jamii ya kiraia ambayo inajumuisha Taasisi au Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Vikundi ya Kiraia na watu binafsi katika kupeleka mbele maendeleo ya nchi zetu na kupambana na matatizo mbalimbali yanayoathiri vibaya maendeleo hayo. Kufunguliwa rasmi kwa Tamasha hili na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein** pamoja na kushiriki kikamilifu kwa wawakilishi mbalimbali wa Serikali katika Tamasha ni kielelezo sahihi cha ushirikiano uliopo na unaoendelea kuimarika baina ya Serikali na Taasisi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Lakini ni vizuri kukumbuka kwamba hali ya ushirikiano baina ya Serikali na NGOs si jambo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu katika bara hili. Na kusema kweli mpaka hivi sasa bado kuna wasiwasi wa hapa na pale.

Hadi miaka michache tu iliyopita haikuwa rahisi kuwa na uhusiano mwema. Palikuwa na shutuma pande zote mbili, kulaumiana pande zote mbili yaani Serikali na Taasisi na Mashirika yasiyo ya Serikali.

Hivi sasa mambo yamebadilika sana ingawa bado hatujafikia kikomo cha uelewano na ushirikiano. Hali halisi katika Afrika na mazingira ya kimataifa yamedhihirisha umuhimu wa ushirikiano huo. Na katika midani ya Bara letu hatua thabiti zimeanza kuchukuliwa kuimarisha ushirikiano. Mapema mwaka jana nikiwa bado Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi za Huru za Afrika tuliitisha Mkutano wa Sekta ya Jamii ya Kiraia ambao licha ya kushirikisha wawakilish wa Taasisi za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pia ulihudhuriwa kikamilifu na wawakilishi wa Serikali za nchi zetu. Hatua kama hiyo haikuwezekana miaka michache iliyopita kwa vile baadhi ya Serikali wanachama wa OAU hawakuwa tayari wawakilishi wao wakae pamoja na wawakilishi wa NGOs katika kikao rasmi kujadili mambo ya bara letu. Mwezi wa Juni mwaka huu OAU pia iliitisha kikao cha Jamii ya

Kiraia kwa sababu ya matayarisho ya kuanzishwa kwa Muungano wa Afrika (African Union). Ninachotaka kusema ni kwamba hali imebadilika na itaendelea kubadilika na ni vizuri sote kwa pamoja tukayatumia vyema mabadiliko hayo ili tuzidi kuimarisha michango ya Taasisi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya nchi zetu za Afrika.

Nimeelezwa kwamba Kongamano lenu limezingatia na kujadili mambo mbalimbali pamoja na mazingira ya ndani na nje ya nchi yetu ambayo kwa namna moja au nyingine yanaathiri jitihada zetu za kupambana na umasikini na kujiletea maendeleo endelevu. Hayo ni pamoja na mikataba au makubaliano mbalimbali ya kimataifa yakiwemo maazimio ya Shirika la Biashara Duniani (WTO) na hasa maamuzi na makubaliano ya Doha, maandalizi ya Mkutano wa Kimataifa juu ya maendeleo endelevu (WSSD) utakaofanyika huko Johannesburg kuanzia mwisho wa mwezi wa Agosti mwaka huu na Ushirikiano Mpya kwa ajili ya Maendeleo ya Afrika (NEPAD). Nimeelezwa kwamba michango na majadiliano kuhusu yote

hayo ilikuwa ya kusisimua. Naamini kuwa mchango wenu utakuwa msaada mkubwa kwa wale wote wanaotuwakilisha. Sina nia ya kuanzisha mjadala mpya. Lakini kutokana na majukumu niliokuwanayo kabla ya kumaliza muda wangu kama Katibu Mkuu wa OAU, ningependa niseme machache kuhusu NEPAD.

Huu ni mpango wa maendeleo ambao umebuniwa, kuzingatiwa, kujadiliwa, kukubaliwa na kuanzishwa na Viongozi wa Afrika kwa lengo la kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika bara letu. Mpango huu unatoa majukumu makubwa zaidi kwetu sisi wenyewe Waafrika. Una lengo la kuimarisha utawala bora, kuimarisha kuheshimu haki za binadamu, kuimarisha ushirikiano katika sekta mbalimbali za kiuchumi kwa lengo hasa la kuifanya karne hii iwe karne ya Afrika. Mpango huu pia unazungumzia ushirikiano au ubia na nchi zilizoendelea ili kufanikisha malengo yetu. Ni muhimu kusisitiza hapa kwamba ikiwa ushirikiano unaotegemewa unapatikana au la, majukumu yetu yapo pale pale. Kwa mfano umuhimu wa kuwa na utawala bora, mfumo wa kidemokrasia, kuheshimu haki za

binadamu, kupambana na rushwa, ushirikiano baina ya nchi zetu au mambo ya wazi na ni mambo ambayo tunayapigania kila siku. Hatuyasisitizi haya kwa kufurahisha wahisani.

Katika miezi kadha tokea mpango huo upitishwe huko Lusaka, Zambia, mwaka jana, kwenye kikao cha Viongozi wa OAU, kumekuwa na malalamiko mbalimbali na hasa Taasisi na Mashirika Yasiyo ya Serikali. Dosari kubwa iliyokuwa ikitolewa ni kwamba uandalizi wa NEPAD haukuwashirikisha vya kutosha walengwa wenyewe – yaani wananchi wa Bara letu. Si rahisi wala si busara kupuuza lalamiko hilo. Ndio maana katika miezi michache iliyopita kumekuwa na juhudi maalum zenye lengo la angalau kupunguza malalmiko haya. Kwa mfano, huko Addis Ababa mwezi Machi mwaka huu na baadae mwezi Juni, mikutano iliofanyika chini ya ECA au OAU iliwapa nafasi kubwa wawakilishi mbalimbali wa NGOs kujadili NEPAD na kutoa dukuduku zao.

Baadhi ya maoni yaliyotolewa yamefanyiwa kazi. Kwa mfano huko Durban kwenye mkutano anzilishi wa Muungano wa Afrika iliwekwa wazi kwamba NEPAD ni chombo cha AU. Lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuhakikisha kwamba wananchi wenyewe wanaiona NEPAD kama ni mpango wao na kwamba baadhi ya malalamiko ya msingi yaliyoanishwa katika vikao mbalimbali yanashughulikiwa. Lakini kazi hiyo haihusu NEPAD tu. Ni muhimu kwa watu wetu wakaelewa fika maana, majukumu na mategemeo ya Muungano wa Afrika na maamuzi mengi mengine ambayo yanaathiri kwa namna moja au nyingine maslahi ya nchi zetu na Bara letu.

Kwa hiyo ni jambo la faraja kuona kwamba Taasisi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na sekta ya Jamii ya Kiraia kwa ujumla yanashughulikia mambo haya. Mwenendo huu uimarishwe. NGOs zetu ziwe na taratibu maalum za kuzingatia, kuchambua na kutoa mapendekezo kuhusu mambo yote na hasa yale ya msingi ambayo yanaathiri kwa namna moja au nyingine uhai na maendeleo ya nchi zetu.

Tamasha hili limefanyika wakati ambapo Bara la Afrika limepania kukabili kwa nguvu mpya vikwazo na sababu zinazopelekea kuvia kwa maendeleo ya bara letu. Nguvu yetu kubwa ni wananchi wa bara letu. Ndiyo maana msisitizo mkubwa umewekwa katika kuimarisha demokrasia na utawala bora katika bara letu. Nia hii maana yake ni kutoa fursa zaidi ya kuwashirikisha wananchi katika kujiletea maendeleo. Ninaamini taasisi mnazoziwakilisha zina nafasi ya pekee katika kuimarisha misingi ya demokrasia shirikishi na utawala bora.

Njia moja ambayo mnaweza kusaidia kujenga utamaduni huu ni kwa taasisi zenyewe kuwa kielelezo sahihi cha demokrasia na mfano bora wa kuigwa wa viongozi kuwajibika kwa wanachama wa taasisi hizi. Ushauri wangu kwenu katika kulifunga kongamano hili ni kwamba turudi katika maeneo yetu ya kazi na kuhakikisha kwamba **tunawajibika ipasavyo na kutumikia kwa uadilifu.**

Ninalisisitiza hili kwa sababu ninaelewa kuwa ni rahisi zaidi kudai demokrasia na uwajibikaji wakati madai hayo yameelekezwa kwa wengine na hususani kwa serikali wakati sisi wenyewe tukiihofia demokrasia. Misingi ya demokrasia lazima ijengwe ndani ya jamii husika ili hatimaye ijidhihirishe kuwa ni utamaduni na mwenendo wa maisha yetu.

Jambo jingine ambalo ningependa kusisitiza ni umuhimu wa kujenga na kuimarisha mtandao unaowezesha taasisi na vyama vyenu kujitambua kuwa wapo washiriki wenzenu katika kutekeleza lengo la kuwahudumia Watanzania. Kuna haja ya kuimarisha mfumo wa kubadilishana mawazo na uzoefu baina ya taasisi zinanofanya vikosi vya jeshi moja. Vita tunavyopigana ni moja ingawa medani zaweza zikawa tofauti. Si vema basi tukatiliana mashaka na kutenda kazi kama vile ni vikosi vya majeshi tofauti. Hali hii isiruhusiwe kuota mizizi kwani inaweza hata kuwachanganya wale tunaokusudia kuwahudumia.

Ni muhimu nikasisitiza vilevile ukweli kwamba taasisi zisizo za kiserikali ni taasisi zisizo za kiserikali. Hizi si idara za serikali bali ni washiriki wenza wa serikali katika maendeleo. Uhuru huu wa taasisi hizi unastahili ulindwe ili kuziwezesha kufanya kazi kama vyombo vinavyojitegemea. Lakini ni vema kusisitiza vilevile kuwa uhuru na kujitegemea huku kusitafsiriwe kuwa taasisi hizi ni badala ya serikali. Ipo haja ya kuanzisha mipango na kugawana majukumu, kubadilishana taarifa za utekelezaji wa mara kwa mara katika ngazi mbalimbali kwa mfano baina ya serikali za vijiji, mitaa au kamati husika za Halmashauri za Wilaya. Kufanya kazi kwa uwazi kiasi hiki kunaweza kusaidia kuondosha hali ya kutiliana mashaka na hivyo kuimarisha mshikamano baina ya wadau wote.

Mipango ya Serikali na mashirika yake au mipango ya Taasisi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali au mipango ya mchanganyiko wa nguvu hizo kwa jumla yanalenga kuboresha hali na maisha ya watu wetu. Ni wazi kwamba mipango yote hiyo na juhudi kemkem zitakwenda kombo ikiwa wale wanaolengwa wanaendelea kuteketea. Ahweni gani itakayopatikana ikiwa

wale waliokusudiwa yaani watu wetu wanaendelea kutoweka? Ugonjwa wa Ukimwi ni hatari na tishio tunaloishi nalo. Sina haja ya kutoa takwimu kuhusu athari kubwa janga hili la ukimwi liliotuletea katika nchi yetu na Afrika kwa jumla. Mamilioni ya watu wetu katika Afrika wameshapoteza maisha yao. Mamilioni ya watoto wetu ni mayatima. Na mamilioni zaidi wameshaambukizwa na kila kukicha janga hili linaendelea.

Kwa hiyo ni jambo lililo dhahiri kuwa mipango yote na jitihada za mashirika yote mnayoyawakilisha itakuwa endelevu ikiwa tutafanikiwa kuzuia au angalau kupunguza kasi ya kuenea kwa maambukizi ya virusi vya HIV na ugonjwa wa AIDS. Kwa hiyo ni vyema pamoja na mambo mengine tujenge utaratibu katika shughuli zetu kukumbushana juu ya umuhimu wa kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya janga la maradhi haya ambayo yanatishia kuvuruga hata yale mafanikio kidogo tuliyopata.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati na pongezi kwa vyama vyote vya hiari na mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yanafanya kazi kubwa kupambana na kuenea kwa ukimwi na

athari za ugonjwa huo kwa jamii. Ukimwi ni vita dhidi ya utu wetu. Ni vizuri tukakumbushana kwamba ugonjwa huu unaweza kumuathiri yeyote yule asiyechukua tahadhari ipasazo. Ukimwi haujui masikini au tajiri, haubagui kwa misingi ya rangi, dini, au kabila na hauheshimu mipaka ya jiografia. Ni vita yetu sote. Ninashauri kwamba kila tunapopata fursa tuitumie fursa hiyo kufikisha ujumbe kwa walengwa wetu, na tuoanishe mipango yetu na mpango wa taifa wa vita dhidi ya ukimwi. Hapo hapo napenda kusisitiza umuhimu wa kuhakikisha kwamba wale ndugu zetu walioambukizwa HIV wanaendelea kupata heshima zote kama raia wengine wote, wasibaguliwe na wapatiwe fursa kikamilifu kuchangia katika maendeleo ya Taifa letu na bara letu.

Ndugu Mwenyekiti na washiriki wa tamasha hili, ninawapongeza kwa kazi nzuri mliyoifanya na nawatakia kila la kheri katika kuwahudumia wananchi wenzetu. Baada ya kusema hayo sasa natangaza rasmi kuwa tamasha la pili la mashirika yasiyo ya kiserikali limefungwa.

Ahsanteni.